



# afya yako
# maisha yako ya baadaye

## Pata Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi

Swahili | Kiswahili




### Mlango wa uzazi ni nini?

Mlango wa uzazi ni sehemu ya mfumo wa uzazi. Iko juu ya uke na huunganisha uke na uterasi (mfuko wa uzazi).

### HPV ni nini?

Virusi vya papiloma ya binadamu (HPV) ni virusi vya kawaida ambavyo hupitishwa kutoka kwa mtu hadi mtu kupitia mawasiliano ya kingono, ikijumuisha kuwasiliana kwa kingono katika kugusana ngozi kwa ngozi. HPV ndiyo chanzo kikuu cha saratani ya mlango wa uzazi.

### Saratani ya mlango wa uzazi ni nini?

Saratani ya mlango wa uzazi ni ugonjwa mkali. **Katika hatua za mapema, kunaweza kusiwe na dalili za wazi.** Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kinaweza kuona mabadiliko ambayo yanaweza kutokeza na kuwa saratani.

**Kipimo hiki kinaweza kuokoa maisha.**

### Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi ni nini?

Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kilibadilisha kwa Kipimo cha Pap Smear. Kinapima kwa HPV na kinafanywa na daktari au muuguzi au unaweza kukifanya wewe mwenyewe.

Kipimo ni cha haraka na **salama**. Wakati mwingine unaweza kujisikia vibaya lakini hakiumizi. Hakiathiri ubikira.

Unaweza:

- kuomba **daktari au muuguzi wa kike**
- kuomba kuwa na **mkalimani**
- kuchukua rafiki au mwenzi/mume.

### Je, unahitaji kupata kipimo hicho lini?

Ikiwa una umri wa miaka 25 au zaidi na umewahi kuwa na mawasiliano yoyote ya ngono, weka miadi na daktari au muuguzi kwa ajili ya kipimo.

Unapaswa **kuwa na Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kila mara baada ya miaka mitano** hadi uwe na umri wa miaka 74. Hata kama majibu ya kipimo chako cha mwisho yalikuwa mazuri, unapaswa kupokea ukumbusho wa kupanga kipimo chako kinachofuatia.

### Chanjo ya HPV ni nini?

Nchini Australia, kuna chanjo ambayo inasaidia kukinga watu dhidi ya HPV.

Wanafunzi wote, kujumuisha wavulana, wa Mwaka wa 7 wanaweza kupata chanjo bure ya HPV. Kama wewe ni mzazi au mlezi, utapokea barua ya kusaini na kurudi shuleni kwako kama ungependa mtoto wako apate chanjo. Chanjo hiyo itasaidia kukinga mtoto wako kutokana HPV wakati anapoanza shughuli za kingono au kuoa au kuolewa.

Ikiwa mtoto wako amekosa kupata chanjo shuleni, anaweza bado kuipata kwa bure hadi anakuwa na umri wa miaka 25. Kama ungependa kuchanjwa kama mtu mzima, uliza daktari wako.

Ikiwa umeshapata chanjo ya HPV bado unahitaji Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kuanzia umri wa miaka 25, kwani chanjo haiwezi kukinga dhidi ya kila aina ya HPV.

Chanjo hii ni salama, haisababishi saratani na haileti matatizo ya kuzaa watoto.

true relationships & reproductive health

Queensland Government

V1-20210513

# Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kinaweza kuokoa maisha.

## Watu wengi wanaopata saratani ya mlango wa kizazi hawajapata kamwe Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi au hawakupata kipimo katika miaka mitano iliyopita.

HARAKA na salama

Tunza afya yako KWA FAMILIA YAKO

## Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kinafanya jinsi gani?

**Una chaguzi mbili.**

Unaweza kukusanya sampuli yako mwenyewe, au daktari wako au muuguzi anaweza kukusanya sampuli yako. Chaguzi zote ni sahihi na salama.


### Mkusanyiko wa Daktari/Muuguzi

Kwa ufaragha unaweza kufunika mwili wako wa chini na shuka.

Daktari au muuguzi anaingiza spekulum ndani uke.

Kisha anatumia brashi ndogo wa laini kuchukua sampuli kutoka kwenye kizazi na kuituma kwenye maabara kwa ajili ya kupima.

Wakati majibu hayo yanakuwa tayari, daktari au muuguzi atawasiliana nawe. Kama sivyo, wasiliana na kliniki ili kupata majibu yako.




Ikiwa unaombwa kurudi kwenye miadi, ni muhimu sana kwamba uhudhurie.

### Kujikusanya


Daktari au muuguzi atakupa usufi na kukueleza kitu cha kufanya.

Unaweza kukusanya sampuli yako katika ufaragha nyuma ya pazia katika chumba cha kliniki, au katika bafuni.

Ondoa sufi kutoka kifurushi na ingiza sentimita chache kwenye uke.

Zungusha usufi kwa sekunde 10 hadi 30, kisha uondoe na weka tena katika pakiti.

Unaweza kuomba daktari wako au muuguzi kwa usaidizi wakati wowote.



Wanawake ambao wamekatwa au kutahiriwa wanaweza bado kuuliza kuhusu kipimo.

PIMA kila baada ya miaka 5

Kinga nzuri sana kuzuia saratani ya kizazi ni kupata **Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kila miaka 5.**

## Je, unaweza kupata Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi bure wapi?

- Kliniki ya Daktari wa Kawaida (GP). Uliza kama wanafanya "kulipwa kwa serikali" (bure)
- Vituo vya Afya ya Jamii
- **Kliniki ya True**- Brisbane, Ipswich, Toowoomba, Cairns na Rockhampton

**Wasiliana na Kliniki ya True Brisbane**

07 3250 0200

clinicreception@true.org.au

**true.org.au/clinic**

Uchunguzi wa Mlango wa Kizazi ni **muhimu**

true relationships & reproductive health

Rasilimali hii imetengenezwa pamoja na Kikundi cha Ushauri wa Afya yenye Kujibu kwa Kitamaduni na mashauriano ya jamii.

Queensland Government

V2-20220118